# Jarida la Mtandao

01 Oktoba, 2025



# ZIARA YA BODI YA WAKURUGENZI YA NHIF MIKOA YA

| Kigoma | Katavi | Rukwa | Songwe | Mbeya |
|---|---|---|---|---|
|  |  |  |  |  |



# BODI YA WAKURUGENZI YA NHIF YAFANYA ZIARA MKOANI KIGOMA

22.09.2025

Katika kuimarisha utendaji wa ofisi za NHIF mikoani, Bodi ya Wakurugenzi imefanya ziara katika Ofisi ya NHIF Mkoa wa Kigoma. Katika ziara hiyo, Bodi ilikutana na watumishi wa ofisi hiyo kwa lengo la kusikiliza na kupitia taarifa ya utekelezaji wa majukumu na shughuli mbalimbali za ofisi.

Mwenyekiti wa msafara huo CPA. Dickson A. Kaambwa ambaye anamwakilisha Mwenyekiti wa Bodi, alitoa pongezi kwa utendaji kazi wa ofisi ya Kigoma na akawahimiza watumishi kuendelea na juhudi ili kufikia malengo. Bodi pia ilisisitiza umuhimu wa kuweka malengo yanayopimika ili kupima mafanikio na changamoto.

Pamoja na pongezi hizo Bodi ilielekeza kupambana na vitendo vya udanganyifu na kuupigania Mfuko dhidi ya watu wanaotaka kuuhujumu. Aidha Bodi ilisisitiza kuongeza juhudi katika maeneo ya usajili wa wanachama na ukusanyaji michango ili kuimarisha zaidi uwezo wa Mfuko.

Akizungumza kwenye kikao hicho Mkurugenzi Mkuu wa NHIF Dkt. Irene C. Isaka, aliwapongeza watumishi wa ofisi ya Kigoma kwa utendaji mzurina akipongeza jitihada zilizofanyika na ofisi hiyo kupata kiwanja kwa ajili ya kujenga ofisi ya Mfuko mkoani hapo.

Dkt. Isaka Alisisitiza dhamira ya Mfuko kuongeza wanachama kwa kuelezea jitihada mbalimbali zunazofanywa ikuwemo kuingia makubaliano na Mrajisi wa vyama vya ushirika ili kusajili wakulima Akielezea fursa nyingine za wanachama mkoani humo kwa ajili ya kuwafikia Dkt. Isaka alitaja makundi ya wajasiriamali, wavuvi na wakimbizi kama maeneo ya kuweka mkazo ili kusajili zaidi. Dkt. Isaka alisema irakuwa vyema kama wakazi wa Kigoma angalau asilimia 10 watasajiliwa ma NHIF, pia alihimiza ofisi ya mkoa kuanzisha ushirikiano na benki mkoani hapo ili kuhamasisha mikopo kwa wanachama wapya.

Vilevile Dkt. Isaka aliwasisitiza watumishi kuhamasisha walimu kusajili wanafunzi, kufanya kazi na mawakala waliopo, na kutumia Wahudumu wa Afya ngazi ya jamii (CHWs) ili kueneza elimu ya bima ya afya miongoni mwa wananchi. Alielezea kuwa menejimenti inaendelea kufuatilia mipango ya kuwasajili kaya zisizo na uwezo ili kufanikisha bima ya afya kwa wote.

Kwa upande wa usimamizi wa fedha na udhibiti wa udanganyifu, Dkt. Isaka aliipongeza ofisi ya Kigoma kwa kuhimiza matumizi ya mifumo ya kielektroniki kwenye vituo vya huduma za afya hali inayosaidia kuthibiti udanfanyifu.

Meneja wa NHIF Mkoa wa Kigoma, Bw. Gwamaka Mwakyoma, akiwasilisha juhudi za ofisi yake katika kutimiza malengo ya Mfuko licha ya changamoto za mwaka uliopita. Alipendekeza kuanzishwa kwa ofisi ndogo Kasulu ili kuboresha huduma na kuongeza usajili wa wanachama.

Alieleza kuwa ofisi ya Kigoma inatoa huduma bora kwa wateja na ina ushirikiano mzuri na taasisi za serikali kama PSSSF, NSSF, TANESCO, TRA na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, hali inayoboresha taswira ya NHIF mkoani humo.

Kuhusu madai, alieleza kuwa vituo vingi vinaanza kutumia mfumo wa kuchakata madai kwa mtandao, japokuwa baadhi bado vina changamoto za miundombinu. Lengo ni vituo vyote kuwa kwenye mfumo kufikia Desemba mwaka huu.









## Kigoma

















# Bodi ya NHIF Yaridhishwa na Utendaji wa Ofisi ya Katavi

Bodi ya Wakurugenzi wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) imeonesha kuridhika na utendaji wa Ofisi ya NHIF Mkoa wa Katavi, baada ya kusikiliza taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya ofisi hiyo. Mwenyekiti wa ziara hiyo CPA Dickson A. Kaambwa, aliipongeza ofisi kwa mafanikio katika eneo la usajili wa wanachama na ukusanyaji wa michango pamoja na huduma kwa wateja, licha ya changamoto kadhaa za kimazingira.

Kwa robo ya kwanza ya mwaka huu wa fedha, ofisi ya Katavi imefanikiwa kusajili wanachama kwa asilimia 71 ya lengo, na kukusanya asilimia 55 ya michango. Hii ni hatua nzuri ukilinganisha na utendaji wa mwaka wa fedha 2024/25. Hata hivyo, bado kuna changamoto ya kufikia malengo kamili ya ukusanyaji michango na utoaji wa huduma.

Pia Bodi ilisisitiza malengo yanayopangwa yawe yanapimika ili wakati wa tathmini iwe rahisi kujua ufanisi wa malengo hayo. Kwa upande wa Udanganyifu, Bodi imeendelea kuweka mkazo kuwa haitavumilia vitendo vya udanganyifu.

Mkurugenzi Mkuu wa NHIF Dkt. Irene C. Isaka, aliwatia moyo watumishi wa Katavi kwa juhudi zao na kuahidi kushughulikia changamoto za vitendea kazi ili kuongeza ufanisi zaidi. Alisisitiza kuweka malengo mahsusi ya kusajili wakulima, wafanya biashara, wanafunzi pamoja na kuhakikisha sekta rasmi inasajiliwa kwa asilimia 100. Alihimiza kushirikiana na Mabenki, mawakala wa bima, vyama vya ushirika, pamoja na Wahudumu wa Afya Ngazi ya Jamii (CHWs). jitihada hizi zitawawezesha kufikia malengo ya Mfuko.

# KATAVI

















23.09.2025



# Ziara ya Bodi ya Wakurugenzi wa NHIF Rukwa: Watumishi Wahimizwa Kuongeza Ubunifu na Kasi ya Utendaji

Bodi ya Wakurugenzi wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) imefanya ziara katika Ofisi ya Mkoa wa Rukwa na kuwataka watumishi kuongeza ubunifu na juhudi katika utekelezaji wa majukumu yao ili kuongeza tija na kufanikisha nia ya Serikali ya kufikia Bima ya Afya kwa Wote.

Akizungumza wakati wa kikao cha tathmini na watumishi wa ofisi hiyo, Mwenyekiti wa msafara Prof. George M. Ruhago, alisema kuwa licha ya jitihada zilizofanywa na ofisi hiyo, bado matokeo yanaweza kuboreshwa zaidi endapo kila mtumishi ataweka ubunifu katika kazi zake za kila siku.

“Tunataka kuona ubunifu ambao unaleta matokeo chanya. Kila mtumishi anapaswa kujiuliza, leo nimefanya nini cha tofauti kinachoongeza thamani kwa wananchi na kwa Mfuko. kujituma na kuwa wabunifu, ndio njia pekee ya kufikia lengo letu la Bima ya Afya kwa Wote,” alisema Prof Ruhago.

Aidha, alisisitiza kuwa malengo yanayowekwa lazima yaweze kupimika ili kurahisisha tathmini ya utekelezaji wake.

Katika eneo la udanganyifu, Prof. Ruhago aliwaagiza watumishi wa Rukwa kuendelea kutafuta njia za kugundua mbinu zinazotumiwa na baadhi ya watoa huduma na wanachama kufanya udanganyifu kinyume na Sheria.

Aidha Mjumbe mwingine wa Bodi CPA Dickson Kaambwa alihimiza kuwa na mipango inayoonesha idadi ya usajili wanachama na ukusanyaji wa michango.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa NHIF Dkt. Irene C. Isaka, alisisitiza umuhimu wa kutumia mifumo ya kidijitali katika kuboresha huduma na kudhibiti mianya ya udanganyifu.

Pia aliwaasa watumishi kuhakikisha wanandikisha angalau asilimia 10 ya wakazi wote wa Mkoa wa Rukwa ili kuongeza wigo wa wanachama.

Vilevile alieleza kuwa ni muhimu kutumia mawakala wa NHIF pamoja na mabenki yanayoweza kutoa mikopo kwa wajasiriamali na wakulima kupitia vyama vya ushirika ili kuongeza idadi ya wanachama. “Lengo letu ni kuhakikisha kila mwananchi anapata huduma bora za afya kupitia bima, na ninyi mko mstari wa mbele kufanikisha hili,” alisema Dkt. Isaka.


















# RUKWA



## NHIF SONGWE YAPONGEZWA KWA USHIRIKIANO NA WADAU, YAHIMIZWA KUSIMAMIA ZAIDI UBORA KATIKA UCHAKATAJI MADAI

Mwenyekiti wa msafara wa Bodi ya Wakurugenzi wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) Prof. George M. Ruhago, akiwa ziarani mkoani Songwe amewataka watumishi wa Ofisi ya NHIF Songwe kusimamia ubora wa uchakataji wa madai ya watoa huduma ili kupunguza malalamiko yanayotokana na makato kwenye madai yanayowasilishwa.

Amesema makato mengi yanaweza kuashiria udanganyifu au ukosefu wa uelewa wa taratibu kwa watoa Huduma.

Prof. Ruhago aliwapongeza kwa juhudi zao na kuwataka kuendelea kujipanga kuelekea utekelezaji wa Bima ya Afya kwa Wote, sambamba na kutumia rasilimali za Mfuko kwa uangalifu ili kuleta tija na manufaa kwa wanachama.

Aidha, Mjumbe wa Bodi CPA Dickson A. Kaambwa aliwasisitiza kuandaa mipango inayopimika ili wakati wa kufanya tathmini waweze kubaini changamoto zinazokwamisha kufikia malengo, huku akiipongeza ofisi kwa mafanikio ya usajili wa waajiri katika mkoa huo.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa NHIF Dkt. Irene C. Isaka, aliipongeza ofisi hiyo kwa kutokuwa na mashauri ya kinidhamu pamoja na ushirikiano mzuri NHIF na taasisi za serikali mkoani humo. Pia aliwataka kutumia wadau mbalimbali kama mabenki, viongozi wa kiimani na kimila pamoja na mawakala na vyama vya ushirika katika kufanikisha Bima ya Afya kwa Wote.

Dkt. Isaka vilebile aliwakumbusha kuhamasisha vituo vya Afya kuchukua mikopo ya vifaa tiba, dawa na majengo ili kuboresha huduma za Afya kwa wanachama.






# SONGWE














24.09.2025



# Ziara ya Bodi Ofisi ya NHIF Mkoa wa Mbeya, Watumishi waelekezwa kuongeza Usajili wa Wanachama

Bodi ya Wakurugenzi wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) imefanya ziara katika ofisi za NHIF Mkoa wa Mbeya kwa lengo la kujionea namna shughuli za ofisi hiyo zinavyotekelezwa pamoja na kubaini changamoto zinazojitokeza ili kuzitafutia suluhu.

Mwenyekiti wa msafara huo, Prof. George M. Ruhago aliwaasa watumishi wa NHIF kutumia fursa zilizopo kuongeza wanachama. Mbeya ni Mkoa Mkubwa kiuchumi na wenye fursa nyingi. Hivyo ni muhimu kutumia fursa hizo kusajili wanachama, alisisitiza Pro. Ruhago.

Hivyo, aliwataka watumishi kuongeza juhudi ili kuleta matokeo chanya. Hapa kuna vyuo vingi, wafanyabiashara wakubwa na wadogo, wakulima pamoja na watumishi wa Sekta rasmi hivyo Bodi inatarajia matokeo makubwa.

Kwa upande wake, Mjumbe wa Bodi, CPA Dickson mwingine wa A. Kaambwa, alisisitiza umuhimu wa malengo yanayowekwa kuwa na vipimo bayana vya ufanisi ili iwe rahisi kufanya tathmini na kubaini kiwango cha mafanikio pamoja na changamoto zilizojitokeza. Hata hivyo, aliwapongeza watumishi kwa jitihada wanazoendelea nazo katika kufanikisha malengo ya Mfuko.

Mkurugenzi Mkuu wa NHIF Dkt. Irene C. Isaka, aliipongeza ofisi hiyo kuendelea kutekeleza majukumu yao na akawataka waendelee kuongeza ufanisi. Pia aliwasisitiza kuimarisha uhamasishaji kwa wajasiriamali, kutumia fursa za majukwaa kama AMCOSS, kushirikiana na benki, na mawakala waliosajiliwa ili kuhakikisha angalau asilimia 10 ya wananchi wa Mkoa wa Mbeya wanajiunga na bima ya afya.

Dkt. Isaka aliwahimiza watumishi kujituma zaidi, akibainisha kuwa utekelezaji wa bima ya afya kwa wote unahitaji matokeo ya haraka, hasa katika mikoa mikubwa kama Mbeya ambayo ni kitovu cha ukanda wa nyanda za juu kusini.

# MBEYA






















## MAELEKEZO YA BODI KWA UJUMLA

1. Tuweke malengo yanayopimika: wakulima wangapi kati ya wangapi? Wanafunzi, wafugaji, wachimbaji, wavuvi, wajasiri amali, nadereva n.k
2. Tathmini ya udanganyifu, kila mkoa ufanye tathmini kuona visababishi vya udanganyifu: mifumo? Kukosekana kwa mafunzo? Udanganyifu upo zaidi kwenye huduma zipi? Kwanini kiwango cha malipo kinaongezeka ilihali vituo ni vile vile? Nini chanzo cha ongezeko?
3. Kujitahidi kusajili walau 10% ya watu waliopo Mkoani
4. kushirikiana kwa karibu na uongozi wa mkoa na Wilaya/ Halmashauri pamoja na wadau wengine
5. Kufanyakazi kwa karibu na waratibu wa afya ngazi ya jamii (Community Health Workers).
6. Menejimenti kuandaa vifurushi kwa ajili ya Wakulima
7. Vifurushi vya wajasiri amali, madereva malori ambao wapo tayari kuchangia 40,000 kwa mwezi kuandaliwa.
8. Kuanda mfumo wa utambuzi wa wananchi wasiokuwa na NIDA hasa wazee, watoto na wakazi wa mikoa ya Pembezoni.
9. Kushirikiana na mawakala wa Bima, mabenki, vyama vya Ushirika kusajili wanachama
10. Kuhamasisha vijiji vyenye (Carbon Credits) kupata kifurushi cha 150,000 kama hatua ya awali (pilot).
11. Kuhamasisha vituo vya afya kuomba mikopo kwa ajili ya dawa, vifaa tiba, ukarabati na vifaa vya vipimo vya kibiolojia (biometric gadgets)
12. Menejimenti kuongeza staff maeneo ya pembezoni hasa Afisa Udhibiti ubora, wahasibu na afisa uanachama.
13. Kupeleka vitendea kazi Katavi na Kigoma
14. Kushiriki vikao/ mikutano mikubwa katika Mkoa/ Halmashauri ili kuhamasisha kuhusu bima ya Afya
15. Mbeya kuna vyuo vingi vya elimu. Ni muhimu kuongeza usajili wa wanafunzi.
16. Kusajili kiasi ambacho kitatufanya tuweze kujitegemea kimkoa badala ya kusaidiwa na mikoa mingine.
17. Mifumo isomane na Manual zilizoandaliwa ili kuondoa malalamiko. Kamati ya ufanisi wa TEHAMA (ICT efficiency) ihakikishe inaondoa malalamiko ya rejections na kuchelewa kutolewa kwa control numbers
18. Kuhakikisha Sekta ya umma imesajiliwa kwa 100%
19. Kuanza mchakato wa ujenzi ili kuepuka kuvamiwa kwa viwanja vya Mfuko.
20. Watumishi kutoa huduma bora kwa wanachama na wadau pamoja na kuepuka vitendo vya udanganyifu.
21. Bodi inawathamini sana na itaendelea kuwapa msaada na uongozi bora kwenye utekelezaji wa majukumu ya Mfuko.

